JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO

Simu/Nukushi Na: 023 - 2614727
Barua Pepe: info@morogoromc.go.tz
Tovuti: www.morogoro.go.tz.
Unapojibu taja:

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P. 166,
MOROGORO.
TANZANIA

Kumb. Na:MMC/S.10/MMC/28/VOL.IV/82 **Tarehe**: 28/04/ 2020

TANGAZO LA KAZI

Kwa mujibu wa Kibali cha Ajira Mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Halmashauri ya **Manispaa ya Morogoro** chenye Kumb. Na. **FA. 170/361/01/209** cha tarehe 01 Aprili, 2020 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro anawatangazia watanzania wenye sifa na ujuzi stahiki kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

MTENDAJI WA MTAA DARAJA LA III - NAFASI 11

SIFA ZA MWOMBAJI:
Awe mwenye Elimu ya Kidato cha nne au sita na aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja wapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA MTAA DARAJA LA III:

(i) Katibu wa Kamati ya Mtaa
(ii) Mtendaji Mkuu wa Mtaa
(iii) Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa
(iv) Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa
(v) Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa
(vi) Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
(vii) Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa
(viii) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote
(ix) Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa na
(x) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

Ajira.co.tz

Scanned with CamScanner

NGAZI YA MSHAHARA

Kwa mujibu wa Ngazi ya Mshahara wa Serikali, yaani TGS B kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI:

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi kwenye Mtaa wowote ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 - 45.
3. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
4. Maombi yote yaambatane na Wasifu wa mwombaji (CV).
5. Maombi ya ambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha (passport size) zilizoandikwa jina la mwombaji nyuma.
6. Testimonials "Provisional Results", "Results Slips", Kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA.**
7. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
8. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho *yaambatanishwe* kwenye barua ya maombi ya kazi.
9. Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa tena.
10. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **11/05/2020 saa 9.30 Alasiri.**
11. Maombi yote yatumwe kwa njia ya **Posta** kwa:-

MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO,
S.L.P 166,
MOROGORO.

Sheilla E. Lukuba
MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

Tangazo hili pia linapatikana kwenye:-

1. **Tovuti ya Halmashauri ya Manispaa – www.morogoro.go.tz.**
2. **Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma – www.ajira.go.tz**

AjiraLeo.com

Scanned with CamScanner